# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

**MUONGOZO WA UWEZESHAJI MAKUNDI MAALUM**

**(Vulnerable Group Planning Framework)**

**MRADI WA KUBORESHA MILKI YA ARDHI**

**(Land Tenure Improvement Project)**

**February, 2020**

**DODOMA**

# MUHTASARI

## *Utangulizi*

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inaandaa Mradi wa Kuboresha Milki ya Ardhi (LTIP) nchini. Lengo la mradi hu ni kuboresha mfumo wa usimamizi wa ardhi na kuongeza usalama wa Milki ya Ardhi kwa wote wanawake na wanaume nchini. Muongozo huu wa unatoa muelekeo wa maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa LTIP utakaohusisha Makundi Maalumu katika Mikoa na Halmashauri mbalimbali mchini. Pia muongozo huu umeandaliwa kwa kuzingatia sera na taratibu za Benki ya Dunia za kulinda Mazingira na Jamii na Sheria na Taratibu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muongozo wa Uwezeshaji wa Makundi Maalumu pia una maelezo kuhusu ushirikishaji wadau walioainishwa wakati wa maandalizi ya Mradi.

**Maelezo ya mradi**

Kwa muhtasari, shughuli za kutekeleza mradi wa kuboresha milki ya ardhi nchini utatekelezwa katika maeneo makuu manne kama yalivyoainishwa katika sehemu zifuatazo:

**Sehemu 1: Kuongeza usalama wa milki za Ardhi**. Katika sehemu hii mradi utasaidia utoaji wa hati milki za kimila, hati milki, leseni za makazi na shughuli nyingine zinazohusiana. Shughuli katika kipengele hiki zitafanyika katika njia ya umoja na shirikishi ili kuhakikisha usawa wa kijinsia, na ulinzi wa haki za makundi yote ikiwa ni pamoja na wanawake, vijana, wawindaji na wakusanyaji, wafugaji, wakulima, n.k. Mikoa mbalimbali na Halmashauri za Wilaya zitahusika katika utekelezaji wa mradi huu ikiwa ni pamoja na: Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Tabora, Geita, Pwani, Mwanza, Shinyanga, Tanga na Morogoro.  Halmashauri za Wilaya ni pamoja na Dodoma (Chamwino), Simiyu (Maswa), Ruvuma (Mbinga), Katavi (Mpanda), Songwe (Songwe) na Momba Vijijini. Sehemu hii itajumusisha kufanyika kwa shughuli mbalimbali ambazo zimeelezwa hapa:

***Sehemu ndogo ya 1.1:*** Kutoa kwa wingi hati milki za kimila za ardhi katika maeneo ya Vijiji. Sehemu hii italenga kuongeza ufanisi katika maeneo ya majaribio ambayo itasaidia katika utekelezaji wa moja kwa moja katika utoaji wa hati milki za kimila. Zoezi hili linahitaji, ufafanuzi wa awali wa mipaka ya Vijiji, mipango ya matumizi bora ya ardhi, ushiriki wa wananchi katika upimaji wa mipaka ya vijiji pamoja na utatuzi wa migogoro na utoaji wa vyeti vya Vijiji.

***Sehemu ndogo ya 1.2****:* Kutoa kwa wingi hati milki na leseni za makazi katika maeneo ya Mijini. Zoezi hili la utoaji wa hati milki mijini litahusisha michakato miwili tofauti yenye matokeo tofauti: mchakato wa urasimishaji utakaozalisha leseni za makazi 1,000,000 na mchakato wa upimaji wa makazi holela utakaozalisha hati milki 1,000,000. Urasimishaji wa ardhi kwa njia ya utoaji wa leseni za makazi utahusisha makubaliano ya maslahi katika kipande cha ardhi husika,

kuandaa masijala ya ardhi ya mijini na utoaji wa leseni za makazi. Vile vile, mchakato wa upangaji na upimaji wa makazi holela na utoaji wa hati milki, utahusisha uzalishaji wa mipango ya urekebishaji makazi ili kuhakikisha inafuata viwango vya chini vya upimaji mijini (upana wa mitaa na njia, upatikanaji wa nafasi za umma kama vile shule na huduma nyingine).

**Sehemu ya 2: kuboresha mfumo wa usimamizi wa taarifa za ardhi nchini**. Kipengele hiki kitajumuisha uboreshaji na usambazaji wa mfumo unganishi wa taarifa za ardhi (ILMIS) katika Mikoa na Halmashauri mbalimbali nchini, maboresho ya mtandao wa jiodesia, upigaji wa picha za anga, uchoraji wa ramani za msingi, na kuanzishwa kwa miundombinu ya utunzaji wa kumbukumbu za kijiografia (NSDI) ili kuimarisha upatikanaji na ufanisi wa huduma za utawala wa ardhi. ILMIS imefanyiwa majaribio na mradi huu utaiboresha na kuiimarisha zaidi, kusambaza mfumo huu katika maeneo ya mradi kwa njia bora ili kufikia sehemu zote za Nchi kwa ajili ya kuboresha taarifa za ardhi. Mfumo ulioboreshwa wa Jiodesia na ramani za msingi utasaidia sio tu shughuli za usajili wa ardhi lakini pia upatikanaji wa ramani za maeneo ambazo zitasaidia katika shughuli za kijamii, kiuchumi na kimazingira. Kipengele hiki kinajumuisha vipengele vidogo vifuatavyo:

***Sehemu ndogo ya 2.1:*** kuboresha na kuusambaza mfumo wa ILMIS katika Miakao na Haamshauri mbalimbali nchini. Sehemu hii itagharamia awamu ya pili uuandwaji wa mfumo ILMIS kwa kuboresha usimamizi wa pamoja wa hati milki za kimila, hati milki, na leseni za makazi, ikiwa ni pamoja na usajili wa awali na shughuli zilizofuatia. Usambazaji wa mfumo wa ILMIS utatekelezwa katika Mikoa 26 ambapo majengo ya ofisi yatajengwa na kuwekewa miundo mbinu itayosaidia utumiaji mfumo wa ILMIS.

***Sehemu ndogo ya 2.2:*** uzalishaji wa ramani za msingi. Kipengele hiki kitagharamia uzalishaji wa ramani za msingi kwa kutumia picha anga zenye ubora wa hali ya juu za hivi karibuni au picha za angani katika maeneo ya mradi na Wilaya ambazo ziko karibu na Wilaya lengwa za mradi ili kusaidia utoaji wa hati milki kwa wingi nchini, mipango ya matumizi bora ya ardhi pamoja na usimamizi wa ardhi.

***Sehemu ndogo ya 2.3:*** Kuimarisha mfumo wa Jiodesia. Kipengele hiki kitasaidia kuanzishwa kwa vituo vya upimaji masaa yote (CORS) pamoja na miundombinu yake na alama za msingi za upimaji zenye ubora zitakazo saidia katika shughuli za upimaji kwa kutumia mtandao wa upimaji unaotumia satelaiti Duniani wenye gharama nafuu katika matumizi na matengenezo.

***Sehemu ya ndogo 2.4:*** Maboresho ya Mifumo ya Uthamini: sehemu hii itahusisha kuandaa ramani ya viwango vya thamani ya ardhi nchini, kuandaa kanzi data ya taarifa za uthamini ambazo zitatumika katika uthamini kwa ajili ya fidia, kodi nk.

**Sehemu ya 3: Kuimarisha uwezo wa Wizara na taasisi zake:** sehemu hii itajumuisha maboresho ya sera, sheria na kanuni za ardhi, kuwajengea uwezo watumishi wa sekta ya ardhi, kuelemisha umma kuhusiana na masuala ya ardhi ili kuboresha utoaji wa huduma za utawala wa ardhi ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa na ujenzi wa ofisi ili kusambaza mfumo wa ILMIS,

na kuimarisha Mabara ya Ardhi na Nyumba. Kipengele hiki kinajumuisha vipengele vidogo vifuatavyo:

***Sehemu Ndogo ya 3.1:*** Maboresho ya sera, sheria na kanuni. Kipengele hiki kitasaidia kuhuisha na kuunganisha Sera, Sheria na Kanuni kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika utawala wa ardhi na usajili. Hii itafanyika kupitia uchambuzi, warsha na ushauri kama itahitajika.

***Sehemu Ndogo ya 3.2****:* Kujenga uwezo kwa watumishi wa sekta ya ardhi. Kipengele hiki kinalenga katika kuwajengea uwezo wadau wote muhimu katika ngazi ya Makao makuu na Halmashauri. Hii itahusisha mafunzo kwa wafanyakazi katika nyanja mbali mbali za maendeleo ya sekta ya ardhi na walio ndani ya mradi. Itafanyika tathmini ili kuona kama kutakuwa na uhitaji wa mafunzo.

***Sehemu Ndogo ya 3.3:*** Kuimarisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba: kipengele hiki kitasaidia uanzishwaji na uendeshaji wa Mabaraza ya Kata ili kuongeza Mabaraza mapya, kuongeza rasilimali watu na fedha kwa mabaraza yaliyopo, kupunguza kesi, kuandaa miongozo katika ngazi ya Vijiji, Kata pamoja kutoa mafunzo na Vifaa.

***Sehemu Ndogo ya 3.4:*** Maendeleo yanayoonekana ya Utawala wa Ardhi: Kipengele hiki kitasaidia katika ujenzi wa majengo ya ofisi katika Mikoa 26 na ukarabati wa Ofisi za Wilaya 12 zitakazotumika kwa ajili ya mfumo wa ILMIS. Pia litajengwa jengo la Kitaifa la kumbukumbu za ardhi. Kipengele hiki pia kitahusika na manunuzi ya vifaa muhimu kwa ajili ya majengo haya na kuhakikisha vifaa kwa ajili ya mtandao vinafungwa katika ofisi hizo. Aidha, mkakati wa utunzaji kumbukumbu utaandaaliwa.

***Sehemu Ndogo ya 3.5****:* Uhamasishaji wa umma ili kujenga uelewa wa mradi: kipengele hiki kinalenga kujenga uelewa mpana wa utawala wa ardhi, shughuli za mradi wa LTIP, Sera zinazohusiana na ardhi, matakwa ya kisheria, na mifumo ya taarifa za ardhi kwa wadau mbali mbali. Maeneo mengine ya utekelezaji itajumuisha maandalizi ya mifumo ya mawasiliano, ufikishaji wa taarifa na kupima uwezo juu ya uelewa wa mifumo ya utawala wa ardhi. Shughuli zingine ni pamoja na mafunzo kuhusu utunzaji wa hati za ulinzi wa usalama (yaani ESMF, VGPF, SEP na RPF) kwa wadau mbalimbali katika ngazi tofauti katika kipindi cha utekelezaji wa mradi.

**Sehemu ya 4: Usimamizi wa Mradi**: katika muktadha huu, kitengo cha uratibu wa mradi (PCU) kimeanzishwa ndani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kazi muhimu zitakazotekelezwa na PCU ni uratibu wa mradi, manunuzi, usimamizi wa fedha, usimamizi wa mazingira na masuala ya kijamii, pamoja na ufuatiliaji na tathmini. Ni muhimu kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara kwani mradi huu ndio mradi wa kwanza unaojitegemea unaofadhiliwa na Benki ya Dunia na kutekelezwa na Wizara. Uwezo uliopo ndani ya Wizara utaimarishwa ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi wenye mafanikio. Aidha, vifaa, ajira na mafunzo vitatolewa na kuboreshwa ili kuongeza uwezo wa Wizara.

**Muongozo wa Mpango wa makundi maalum**

Muongozo wa Mpango wa makundi maalum umezingatia vipengele mahususi vya sheria za Tanzania na muongozo wa kimazingira na kijamii wa Benki ya Dunia (ESF). Kanuni tisa za viwango vya kimazingira na kijamii (ESSs) vilivyopo katika muongozo wa Benki ya Dunia vinatumika katika Mradi. Kanuni namba 7 (ESS7) inahusu jamii za asili Kusini mwa Jangwa la Sahara, zenye historia ya kitamaduni na ambazo zimekuwa zikipunjwa kimaslahi. Kiwango hiki ESS7, kinahitaji mradi kuongeza fursa kwa makundi maalum ya jamii hizo kushiriki na kufaidika na maendeleo ya mradi kwa njia ambayo haitaathiri mila na desturi zao. Muongozo wa Makundi Maalumu unatoa maelekeo ya kushirikisha Makundi Maalum katika kuendeleza na kutekeleza mradi huu katika ngazi ya jamii.

Kwa mujibu wa Kanuni namba 7a (ESS7), nchini Tanzania Makundi maalumu yanajumuisha jamii za Wafugaji na Wawindaji, ikiwa ni pamoja na Hadzabe, Akie, Sandawe, Maasai na Barbaig. Muongozo huu umeandaliwa kuongoza utekelezaji wa mradi katina maeneo ya makundi hayo ambayo hupatikana kwa kiasi kikubwa Kaskazini mwa nchi ya Tanzania.

Faida kuu ni kuongezeka ulinzi katika makundi hayo kuhusiana na masuala ya haki za ardhi pamoja na rasilimali asilia za ardhi ikiwemo maji, misitu, ardhi ya malisho pamoja na urithi kitamaduni. Aidha, pale ambapo upangaji wa matumizi ya pamoja utafanyika upo umuhimu wa kuainisha na kulinda njia za Mifugo. Faida hizi zitapatikana vizuri zaidi kupitia utoaji wa hati miliki za kimila na uandaaji wa sheria ndogo zinazohusika. Kupitia Elimu na kampeni ya uhamasishaji ufahamu wa makundi maalum na haki zinazohusiana na ardhi utaongezeka na hivyo kuwawezesha kulinda haki zao. Pia, ushirikishaji wa kijiji katika mahitaji yao ya ardhi na utaratibu wa mipango vinaweza kusaidia kupunguza migogoro juu ya upatikanaji wa ardhi.

Muongozo wa Mpango wa makundi Maalum (VGPF) unaonesha athari na hatari kwa makundi maalum pamoja na aina ya hatua zinazohitajika kutekelezwa ili kukabiliana nazo.Hatua hizo zimewekwa kwenye jedwali hapo chini. Hatua hizo zimebuniwa kuangalia hatua za kukabiliana na athari za ukandamizaji na kutengwa kwao; na kuhakikisha kuwa kuna uelewa wa kutosha wa mradi na utekelezaji sahihi unaohusisha wadau wote. Aidha, wakati wa maandalizi ya mpango wa makundi maalum (VGP) hatua hizo zitajadiliwa na makundi husika na iwapo hatua za nyongeza zitahitajika basi zitajumuishwa ili kuwa na matokeo mahsusi ya vipengele vya mradi.

**Athari za Mradi wa Maboresho ya Milki na Njia za Utatuzi**

| **Athari** | **Mapendekezo ya Utatuzi** |
|---|---|
| Kutengwa kwa Makundi Maalum katika hatua za Mradi | • Kufanya uhakiki (kwa kushirikiana na Benki ya Dunia) wa uwepo wa Makundi Maalum katika eneo la mradi.<br>• Kutekeleza Mpango wa Makundi Maalum kwenye maeneo ya mradi yanapopatikana makundi hayo.<br>• Kufanya Uhamasishaji na kuongeza ufahamu kulingana na muongozo wa usimamizi wa makundi maalum katika utekelezaji wa mradi. |

| | |
|---|---|
| | • Kuhakikisha Mikutano yote inatangazwa kwa wakati na kuzingatia muda unaopangwa ili kuruhusu makundi maalum kushiriki.<br>• Kuhakikisha makundi maalum yanaweza kuingiza mawazo kwa kuangalia uhusishwaji wake unaohitajika. |
| Kutokuwepo usawa kunakowakabili Wanawake na Makundi mengine | • Kufanya Uhamasishaji na kuongeza ufahamu kwa Viongozi wa Kimila kwa kujumuisha wanawake na makundi maalum mengine wakati wa mchakato.<br>• Kufanya majadiliano na makundi mbalimbali yaliyotengwa ili kuwajengea ufahamu kuhusu mradi na mchango wa makundi na asasi za kijamii.<br>• Kuelimisha wanaume na wanaumekuhusu umuhimu wa kumshirikisha mwanamke kwenye hati miliki za ardhi.<br>• Kuhakikisha kuwa mwanamke anaweza kuitumia hati katika shughuli za kiuchumi za wanawake.<br>• Kuweka Masuala ya kijinsia katika haki za ardhi. |
| Ukosefu wa ardhi ya umiliki wa pamoja kwa msimu | • Kama sehemu ya Mpango wa Makundi Maalum, kutafanyika ukusanyaji wa taarifa za malisho, maeneo ya ufugaji na mabadiliko ya majira/msimu ili kubainisha matumizi halisi ya ardhi.<br>• Kujumuisha mabadiliko ya misimu na sharia ndogondogo za vijiji katika mipango ya matumizi ya ardhi za vijiji.<br>• Kufanya Uhamasishaji kwa kushirikiana na makundi maalum na jamii kwa upana wake kuhusiana na matumizi ya ardhi ya msimu na kufahamu ushindani wa haki za ardhi na umuhimu wa suluhisho lake.<br>• Utoaji wa Hati za Umuliki wa Ardhi wa pamoja. |
| Haki za Umiliki wa Ardhi wa Pamoja ndani ya Mipaka ya Vijiji | • Kama sehemu ya Mpango wa Makundi Maalum, kutafanyika ukusanyaji wa taarifa za malisho, maeneo ya ufugaji na mabadiliko ya majira/msimu ili kubainisha matumizi halisi ya ardhi ndani ya mipaka ya vijiji.<br>• Kushiriki katika uandaaji wa mipango ya pamoja ya matumizi ya ardhi ya vijiji.<br>• Kuhakikisha kwamba makundi maalum yanashiriki katika uandaaji wa mipango ya pamoja ya matumizi ya ardhi ya vijiji, Sheria ndogondogo na katika maamuzi.<br>• Utoaji wa Hati za Umuliki wa Ardhi wa pamoja. |
| Kushindwa kutumia ardhi za kimila au zinayotokana na kurithi | • Kama sehemu ya Mpango wa Makundi Maalum, kutafanyika ukusanyaji wa taarifa za malisho, maeneo ya ufugaji na mabadiliko ya majira/msimu ili kubainisha matumizi halisi ya ardhi ndani ya mipaka ya vijiji.<br>• Kuandaa Mpango wa makundi maalum katika maeneo ya mradi yanapopatikana makundi hayo.<br>• Kufanya Uhamasishaji na kuwajengea ufahamu makundi maalum kuhusu mradi. |
| Kutwaa Ardhi | • Kuanisha na Kutekeleza hatua zilizoainishwa ndani ya Muongozo wa Uhamishaji wa mradi. |

| | |
|---|---|
| | • Kwa namna itakavyohitajika kutekeleza hatua zilizo ainishwa ndani ya Muongozo wa Mashirikiano na uwazi kwa wadau (FPIC). |

## Ushiriki wa Wadau.

Utayarishaji wa mradi wa Maboresho ya Milki ulitokana na mashauriano na ushirikishwaji wa wadau mbalimbali uliofanywa na Wizara. Wadau hawa ni pamoja na na Asasi zisizo za kiserikali (CSOs), Makundi Maalum na Wataalamu kutoka Taasisi mbalimbali za serikali. Wadau hawa walishiriki kwa njia mbalimbali zikiwemo kutembelea maeneo husika, barua pepe, kufanya mikutano na kwa njia ya mawasiliano ya simu. Mashauriano haya na wadau yalitumika kupata maoni yaliyosaidia kuandaa muongozo na namba ya utekelezaji wake.

**Ushirikishwaji wakati wa Utekelezaji**

Makundi maalum yataarifiwa na kushiriki maandalizi ya mpango wa makundi maalum wakati wa utekelezaji mradi. Ushiriki katika mpango utawawezesha kufaidika kutokana na mradi, kuzilinda haki za makundi haya na kuepuka athari hasi. Mpango wa makundi maalum utatayarishwa kwa ushirikishwaji na kukubalika kwa jamii ya makundi haya kabla ya utekelezaji wake. Katika mchakato huu yafuatayo yatazingatiwa:

a) Angalizo maalum litatolewa katika masuala ya kimila, wanawake, vijana, watoto pamoja na upatikanaji fursa za maendeleo na faida;

b) Kuanzisha mfumo unaofaa wa kijinsia na wa kawaida utakaotoa fursa kwa mashauriano katika kila hatua ya maandalizi ya mradi na utekelezaji miongoni mwa makundi maalum, kama yatakuwepo, na kushirikisha Asasi za kiraia katika maeneo yatakayoathirika kijamii.

c) Kuyapa makundi maalum taarifa zote muhimu kuhusu mradi (ikiwa ni pamoja na tathmini ya athari hasi za mradi katika jamii kwa njia sahihi kwa kila hatua ya Utekelezaji wa mradi.

Ushiriki wa Makundi Maalum katika utambuzi na ufumbuzi wa matatizo ya jamii utazingatiwa wakati wote wa maisha yote ya mradi.

**Njia za Ushirikishwaji wa Makundi Maalum wakati wa Utekelezaji wa mradi**

Ili kupata imani ya utekelezaji wa mradi wa Kuboresha Milki, Wizara kupitia Kitengo cha Uratibu itazingatia ushiriki wa makundi maalum kwa kutumia njia mbalimbali. Njia hizi za ushirikishwaji ni pamoja na kuitisha mikutano kupitia mfumo rasmi wa serikali ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha viongozi wa vijiji, kata na. Njia nyingine ni pamoja na uhamasishaji wa jamii, kushirikisha wadau, kufanya ufuatiliaji, kushirikisha makundi maalum ambapo asasi za kiraia na makundi ya kijamii yatahusishwa kwa makubaliano maalum ambapo makundi hayo yatapaswa kutoa taarifa za mara kwa mara kwa Kitengo cha Uratibu wa Mradi (PCU) na timu ya utekelezaji kulingana na shughuli watakazokuwa wanafanya,, ushirikishwaji wao wa makundi maalum matokeo waliyopata kutokana na ushirikishwaji na mambo mengine yatakayojitokeza kwa ajili ya kuboresha ufanisi.

Timu za mradi na asasi za kiraia zitakaa kwa pamoja na kuangalia ushiriki wa makundi utakaohusisha wadau ili kuhakikisha unafanya kazi. Utambuzi wa mapema wa kutengwa au ukosefu ushiriki katika mchakato huu utakuwa muhimu kuhakikisha mipango inayoidhinishwa inakuwa na mawazo au mapendekezo yao.

Kuhusiana na taasisi, sera na mifumo ya kisheria, Katiba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 inatambua haki za kijamii na za kitamaduni za raia wote kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 8 (2), 9 na 29. Inatambua Makundi Maalum kuwa ni jamii ya wachache iliyotengwa kwa sababu za kihistoria, kijamii, kiuchumi na kwa hivyo, matakwa yao na mahitaji yanapaswa kusikilizwa na kulindwa. Katiba hii pia inakataza kutengwa kwa makundi maalum kwa sababu ya aina yoyote ikiwemo kutoshiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi za nchi yao. Hivyo, haja ya kutambua, kulinda na kuhifadhi utamaduni wa jamii hizi ni muhimu kulingana na kanuni za kimazingira na kijamii (ESS7) ya matakwa ya Benki ya Dunia.

**Mpango wa Makundi Maalum (VGPs)**

Mpango wa Makundi Maalum utaandaliwa wakati wa utekelezaji wa mradi katika halmashauri za wilaya ambapo ushirikishwaji unategemewa kuwa katika kiwango cha juu. Utekelezaji wa Muongozo wa Usimamizi wa Makundi Maalum utasaidia makundi maalum kujenga fursa za kuboresha maisha na ustawi. Mpango wa Makundi Maalum utaandaliwa katika mradi na utajumuisha maudhui yafuatayo:

a) Muhtasari wa mfumo wa kisheria na kitaasisi unaoendana na Makundi Maalum.

b) Taarifa za msingi kuhusu idadi ya watu, jamii, tamaduni, na mazingira ya siasa kwa jamii za makundi maalum husika, ardhi na mamlaka zake ambazo tangu asili wanamiliki au kutumia na maliasili wanazotegemea.

c) Muhtasari wa tathmini ya kijamii inayotoa uchambuzi wa mazingira ya kiuchumi na kitamaduni kuhusiana na makundi maalum.

d) Muhtasari wa matokeo ya mashauriano ya wadau na makundi maalum uliofanyika wakati wa maandalizi ya mradi.

e) Muongozo wa kuhakikisha mashauriano ya awali na makundi maalum kabla ya wakati wa matayarisho na wakati utekelezaji wa mradi na ushahidi wakati wa ukamilishaji.

f) Mpango wa hatua za utekelezaji kuhakikisha kuwa makundi maalum yanapata faida za kijamii na kiuchumi ambazo ni stahiki kitamaduni ikijumuisha pale inapolazimu hatua za kujenga uwezo wa taasisi zinazotekeleza mradi.

g) Pale ambapo athari kubwa kwa makundi maalum zinabainishwa, mpango wa hatua stahiki utatekelezwa ili kuepuka, kupunguza, kushughulikia au fidia athari hizo kwa kutumia taarifa zilizozopo katika muongozo wa kimazingira na kijamii na muongozo wa usimamizi wa makundi maalum wa Benki ya Dunia.

h) Makadirio ya gharama na mpango wa makundi maalum; kila mradi utakuwa na gharama kamili ya kusaidia makundi maalum.

i) Kuwepo na taratibu sahihi katika mradi za kushughulikia Makundi Maalumu yatakayoathirika kutokana na utekelezaji wa mradi. Wakati wa kuandaa taratibu za malalamiko, serikali itaweka taratibu za kimahakama kushughulikia migogoro ya kimila baina ya makundi maalum.

j) Taratibu na viwango stahiki vya ufuatiliaji, upimaji matokeo na kutoa taarifa katika utekelezaji mpango wa makundi maalum. Utaratibu upimaji na ufuatiliaji utajumisha mashauriano ya wazi ya makundi maalum.

Mara baada ya kutayarisha, mpango wa makundi maalum utawekwa wazi na Wizara ya Ardhi kwa wadau wa ndani ikiwa ni pamoja na makundi maalum katika maeneo maalum kwa utaratibu, lugha na njia inayoeleweka na kufikika. Hatua hiyo itajumuisha mikutano na makundi maalum kujadili maudhui ya mpango huo pamoja na viongozi wa kijiji na wafanyakazi husika katika ngazi ya wilaya na mkoa. Nyaraka pia zitakuwa wazi katika tovuti za Benki ya Dunia na Wizara.

**Tathmini na Ufuatiliaji**

Ni muhimu kwamba mpango wa Tathmini na Ufuatiali uandaliwe kwa kushirikisha kikamilifu makundi maalum katika hatua za awali za maandalizi ya mradi kuja na hatua za kukabiliana na athari za kitamaduni katika muktadha huo. Utekelezaji wa Muongozo wa Makundi maalum na mpango wa makundi maalum unapaswa kufuatiliwa kwa karibu na kuwekwa kimaandishi.

Kamati ya Wataalam wa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Kitengo cha Uratibu wa Mradi (PCU) itaangalia jinsi mradi utakavyozingatia mipango ikiwemo tathmini ya kijamii, muongozo wa usimamizi ya makundi maalum, katika hatua za ushirikishwaji unaohusisha makundi maalum. Taarifa za tahmini na ufuatiliaji kwa kila hatua ya mradi zitaandaliwa kwa mwaka zikijuisha taarifa za makundi maalum, na zitaonesha hatua zilizochukuliwa katika kurekebisha mipango wa makundi maalum. Taarifa maalum zilizoainishwa katika mchakato wa tathmini na ufuatiliaji na hatua zitakazochukuliwa zijadiliwe na makundi maalum ili kuendelea kuwa na taarifa na kuhakikisha usahihi wa hatua za marekebisho. Taarifa ya tathmini na ufuatiliaji itawasilishwa kwenye Wizara ya Ardhi na hatimaye Benki ya Dunia kama inavyotakiwa.

**HUU NI MUHTASARI TU WA MUONGOZO WA UWEZESHAJI MAKUNDI MAALUM**

ANDIKO ZIMA LINAPATIKANA KUPITIA:-

**Tovuti: www.lands.go.tz**

KWA MAONI NA USHAURI TUMA KUPITIA:-

**Barua pepe: wakuru.maseka@lands.go.tz, lucy.kabyemera@lands.go.tz, Mariam.silim@lands.go.tz**

**Simu/ Ujumbe wa simu: +255767322277, +255713278040, 0683214181**

Anwani: **Katibu Mkuu**

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

S.L.P 2908.

**Dodoma.**